

Kwanini Mungu alimfunga tumbo Raheli, ilihali Yakobo alimtesekea
miaka 14?

Jibu: Hakuna kosa lolote Raheli alilolifanya, lililomfanya afungwe tumbo asizae.. Lakini tukisoma maandiko twaweza kuona sababu kama mbili zilizopelekea yeye kufungwa tumbo na MUNGU mwenyewe.

1. KUMNYENYEKEZA RAHELI na KUMTIA NGUVU LEA.

Tunasoma kuwa Lea ndiye aliyekuwa wa kwanza kuzaliwa, na Yakobo alimpenda zaidi Raheli kuliko Lea, (*na jambo hilo lilikuwa wazi linaonekana*) kwahiylo labda ingetokea Yakobo aliyebeba ahadi za MUNGU kumuoa Raheli, na tena akazaa naye mtoto wa ahadi, huenda jambo hilo lingemfanya Raheli kujivuna/kujigamba mbele ya Lea dada yake, na hivyo Lea angekuwa duni/mnyonge mbele ya mdogo wake, kwahiylo MUNGU akamfunga tumbo.

*Mwanzo 29:28 "Yakobo akafanya hivi, akatimiza siku zake saba.
Naye akampa Raheli binti yake kuwa mkewe.*

*29 Labani akampa binti yake Raheli mjakazi wake Bilha, awe
mjakazi wake.*

*30 Akaingia kwa Raheli naye, AKAMPENDA RAHELI KULIKO LEA,
akatumika kwa ajili yake miaka saba mingine*

Kwanini Mungu alimfunga tumbo Raheli, ilihali Yakobo alimtesekea
miaka 14?

31 *Bwana akaona ya kwamba Lea hakupendwa, naye akafungua tumbo lake; bali Raheli alikuwa hazai.*

32 *Lea akapata mimba akazaa mwana, akampa jina lake, Reubeni, maana alisema, Kwa kuwa Bwana ameona teso langu; sasa mume wangu atanipenda.*

33 *Akapata mimba tena akazaa mwana, akasema, Kwa kuwa Bwana amesikia ya kwamba mimi sikupendwa, amenipa na huyu; akamwita jina lake Simeoni.*

34 *Akapata mimba tena, akazaa mwana, akasema, Basi wakati huu mume wangu ataungana nami, kwa sababu nimemzalia wana watatu. Kwa hiyo akamwita jina lake Lawi.*

35 *Akapata mimba tena, akazaa mwana. Akasema, Mara hii nitamsifu Bwana; kwa hiyo akamwita jina lake Yuda; akaacha kuzaa”.*

2. KUKITHAMINISHA KITAKACHOZALIWA BAADAYE.

Hii ni sababu ya pili ya Raheli kufungwa tumbo: Tunasoma ijapokuwa Raheli alifungwa tumbo muda mrefu, lakini ulifika wakati akazaa, na

Kwanini Mungu alimfunga tumbo Raheli, ilihali Yakobo alimtesekea miaka 14?

mwana aliyemzaa alikuwa wa tofauti na wale wengine 10 waliotangulia, kwani ndiye aliyekuwa YUSUFU, ambaye alikuja kuwa Mkuu zaidi ya ndugu zake wote, na tena Mkuu juu ya nchi yote ya Misri, baada ya Farao.

Ikifunua kuwa si kila kinachochelewa kina laana!.. Vingi vinavyochelewa ni kwasababu ya Utukufu wake, hivyo usimwone mtu kachelewa kupata mimba ukamdhara!.. Hujui atakayekuja kumzaa ni nani!..

Vile vile usihuzunike unapoona unachelewa kupata mtoto, kwani vizuri na vya thamani, vina gharama, na gharama yenewe yaweza kuwa fedheha, matusi, kejeli na masimango.. Lakini vinavyokuja baada ya gharama hizo vinakuwa ni vizuri, endapo tu utazidi kusimama katika imani, haijalishi muda, vitatokea tu!.

*Wagalatia 4:27 “Kwa maana imeandikwa, Furahi, wewe uliye tasa, usiyezaa; Paza sauti, ulie, wewe usiye na utungu; Maana watoto wake aliyeachwa pekee ni wengi Kuliko wa huyo aliye na mume”.
Bwana akubariki.*

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Kwanini Mungu alimfunga tumbo Raheli, ilihali Yakobo alimtesekea
miaka 14?

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako
bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge
na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

**Kwanini Raheli aliiba miungu ya Baba yake, (Labani) Mwanzo
31:19.**

**Kwanini Labani aseme Yakobo ni Mfupa wake na nyama
yake?(Mwanzo 29:14)**

Raheli aliwalilia vipi watoto wake?

Zeri ya Gileadi ni nini?

Kwanini Mungu alimfunga tumbo Raheli, ilihali Yakobo alimtesekea
miaka 14?

Tunguja ni nini katika biblia? (Mwanzo 30:14).

Share on:

WhatsApp